YALIYOMO

Hotuba ya Mwenyekiti wa Baraza 2
Hotuba ya Makamu Mkuu wa Chuo 10

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili na Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Al-Haj Dk Ali Hassan Mwinyi,

Katibu Mkuu, Wizara Ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Profesa Sifuni Ernest Mchome,

Katibu Mkuu Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Dk. Donan Mmbando,

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Profesa Ephata Kaaya,

Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Muhammad Kambi Bakari,

Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu na Wakuu wa Vyuo Vikuu Vishiriki Mlioko hapa,

Wajumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili,

Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika mbalimbali ya Kimataifa,

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Profesa Lawrence Museru,

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Taasisi ya Mifupa Muhimbili, Dk Othman Kiloloma,

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Dk Diwani Msemo,

Viongozi wa Serikali,
Wageni waalikwa,
Maprofesa na Wahadhiri,
Wahitimu,
Wazazi na Walezi,
Jumuiya ya Wanachuo,
Mabibi na Mabwana,

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Ni furaha yangu kubwa kwa niaba ya Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Uongozi wa Chuo na Wanajumuia wote wa Chuo kuwakaribisheni nyote kwenye maadhimisho ya mahafali haya ya tisa ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili.

Kipekee kabisa natanguliza shukrani zangu kwako Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, kwa kuwa nasi leo na kukubali kuwatunukia stashahada na shahada mbalimbali wahitimu wetu leo.

Aidha napenda kuwakaribisha wazazi, walezi, ndugu, jamaa na marafiki wa wahitimu, bila kuwasahau viongozi mbalimbali wa Serikali, Mabalozi, pamoja na Viongozi wa taasisi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk John Pombe Joseph Magufuli na Makamu wa Rais Mhe Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuongoza Serikali ya awamu ya tano. Tunawatakia baraka za Mwenyezi Mungu katika kutekeleza jukumu hili zito la kuongoza taifa letu.

Pili napenda Kumpongeza Mhe Majaliwa Kassim Majaliwa, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa awamu ya Tano, na vile vile kuwapongeza mawaziri wote walioteuliwa katika nyadhifa zao. Kipekee napenda kumpongeza Waziri wa wizara yetu mama ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kuteuliwa kuongoza wizara hii.

Napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza aliyekuwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo – Utawala, Fedha na Mipango Prof. Muhammad Kambi Bakari kwa kuteuliwa kuwa Mganga Mkuu wa Serikali. Uteuzi huu unaongezea sifa Chuo hiki kwa vile unaonyesha kuwa Serikali inatambua mchango wa wanataaluma na viongozi wa Chuo hiki katika maendeleo ya Taifa hususani sekta ya Afya.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Katika kuimarisha dhana ya utawala shirikishi, Chuo kina utaratibu wa kubadilisha uongozi wa ngazi mbalimbali za utendaji kila baada ya miaka mitatu. Kutokana na hilo basi napenda kuwapongeza Wakuu wa Skuli, Wakurugenzi na Wakuu wa Idara waliochaguliwa kuwa viongozi kuanzia mwaka huu wa masomo kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo. Ni matumaini yangu kwamba mtafanya kazi yenu kwa juhudi na weledi mkubwa ili kutekeleza mikakati na kufikia malengo ya Chuo hiki.

Nichukue nafasi hii pia kuwashukuru Wakuu wa Skuli, Wakurugenzi na Wakuu wa Idara waliomaliza muda wao kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kipindi chote walichokuwa madarakani.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Naomba nichukue nafasi hii vile vile kuwapongeza wahitimu wote wa mwaka huu kwa kufaulu masomo yao na kutuwezesha sisi sote kusherehekea siku ya leo. Kipekee kabisa napenda kutoa shukrani zangu za dhati na pongezi kwa Maprofesa, Wahadhiri pamoja na wafanyakazi wote wa Chuo kwa michango yao iliyowezesha kupata wahitimu hawa.

Napenda pia kutoa shukrani zetu za dhati kwa Serikali, mashirika ya ndani na nje ya nchi, Vyuo Vikuu washirika wetu wa ndani na nje ya nchi pamoja na watu binafsi kwa michango yao ambayo imekiwezesha Chuo hiki kutekeleza majukumu yake katika nyanja za ufundishaji, utafiti na kutoa huduma kwa jamii. Sherehe ya leo ni uthibitisho dhahiri wa mchango wao mkubwa katika utekelezaji mzuri wa majukumu ya Chuo.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Ili kutekeleza kwa vitendo Dira ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inayosisitiza kupatikana kwa mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi,

umahiri, uwezo na mitazamo chanya ya kuweza kuchangia katika maendeleo ya taifa, Chuo kimeendelea kutekeleza mitaala inayosisitiza uwezo wa kutekeleza kwa vitendo (*competency based curricula*). Nina matumaini makubwa kwamba wahitimu wetu wametayarishwa vizuri katika kufikia dira hii.

Hivyo napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa sera hii nzuri ambayo endapo utekelezaji wake utafanyika kama ilivyoainishwa katika matamko ya sera hii, itawezesha kumpata mtanzania katika ngazi zote za elimu, mwenye uwezo wa kuchangia kikamilifu katika kuleta maendeleo ya taifa.

Ni wazi sera hii ikitekelezwa kama ipasavyo itaongeza pia idadi ya wanafunzi wenye sifa za kujiunga na vyuo vya elimu ya juu hasa katika masomo ya Sayansi.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Ili kukiwezesha Chuo kutekeleza vizuri sera hii ya Elimu, napenda kukutaarifu Mheshimiwa Mkuu wa Chuo kuwa, Chuo kinatekeleza mikakati mbalimbali itakayokiwezesha kupokea idadi kubwa ya wanafunzi wenye sifa za kujiunga na Chuo mojawapo ikiwa ni mradi wa ujenzi wa Kampasi kuu ya Mloganzila. Kampasi hii itakapomalizika Chuo kitaweza kuongeza idadi ya jumla ya wanafunzi kutoka 3500 waliopo sasa na kufikia wanafunzi zaidi ya 15,000.

Hivyo napenda nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kuuipa kipaumbele mradi huu wa ujenzi wa Kampasi kuu ya Chuo, Mloganzila. Kwa sasa ujenzi na upatikanaji wa vifaa tiba vya hospitali ya kufundishia uko katika hatua za mwisho za kukamilika. Tunategemea hospitali kuanza kutumika mwezi Juni 2016. Hata hivyo bado tuna changamoto ya upatikanaji wa fedha za ujenzi wa majengo mengine muhimu ya Chuo ili kufanikisha utendaji kazi kwa ufanisi. Ni matumani yetu kwamba Serikali itatoa upendeleo maalum katika vipaumbele vyake

ili ujenzi wa Kampasi hii uweze kukamilika mapema iwezekanavyo, ili kutoa fursa kwa wanafunzi wengi zaidi wenye sifa ya kujiunga na chuo, kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Sera ya Elimu na Mafunzo pia imeweka msisitizo katika kuweka mfumo nyumbufu wa elimu na mafunzo ili kuwezesha wananchi wengi zaidi kujielimisha na kuwa huru kutafuta elimu katika fani wanayoipenda hadi kufikia upeo wowote kulingana na stahili na uwezo wao. Hili ni suala zuri sana katika kuendeleza elimu nchini. Chuo hiki hakiko nyuma katika utekelezaji wa sera hii kwani juhudi mbalimbali zimefanyika katika kuongeza vigezo vya kujiunga na Chuo hiki ili kuwawezesha wahitimu wa fani za afya katika ngazi mbalimbali kujiunga na elimu ya juu. Ni mategemeo yetu kuwa Chuo kitachangia kwa kiasi kikubwa katika upatikanaji wa wahitimu wa afya katika fani mbalimbali wanaohitajika katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now*) wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hauwezi kufanikiwa bila juhudi za makusudi za kuongeza rasilimali watu kwenye sekta ya afya katika ngazi zote na kuwaendeleza wale walio kazini katika kupata elimu ya kijiendeleza katika utendaji kazi wao.

Ili kuendana na mpango huu, Chuo kimeweka mikakati kadhaa ikiwemo ya kuongeza idadi ya udahili wa wanafunzi katika programu na ngazi mbali mbali. Ili kufanikisha lengo hili, jengo lililojengwa na Chuo kuendeshea mafunzo kwa ajili ya watumishi wa sekta ya afya katika ngazi zote limekamilika. Hii itakiwezesha Chuo kuchangia kikamilifu katika mpango huu.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Pamoja na nia nzuri na ya dhati kabisa ya Chuo kuchangia katika kufikia malengo ya sera mbalimbali zilizowekwa na Serikali ili kuleta maendeleo kwenye sekta ya afya na elimu nchini, Chuo kinakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha za kutosha kuendeshea shughuli zake. Ingawa Chuo kimeweka mikakati na sera mbalimbali za kuongeza vyanzo vya mapato ya ndani, bado mapato hayo hayajafikia kiwango cha kuendesha shughuli zake kwa ufanisi mkubwa bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini.

Kati ya changamoto kubwa zinazokikabili Chuo katika Kampasi ya Muhimbili ni uchakavu na ufinyu wa miundo mbinu. Majengo mengi ya Kampasi hii yalijengwa miaka ya sitini na nafasi ya upanuzi haikuwezekana ili iendane na ongezeko la udahili wa wanafunzi. Kwa mfano kati ya wanafunzi walioomba kukaa katika mabweni ya chuo kwa mwaka huu, wanafunzi mia tano hawakupata nafasi kutokana na mahitaji kuwa makubwa kuliko nafasi zilizopo. Vile vile mwaka jana na mwaka huu Chuo kilidahili wanafunzi wengi zaidi na hivyo kukabiliwa na msongamano katika mabweni, madarasa na maabara. Ongezeko hili la udahili ambalo limesababishwa na ongezeko la ufaulu katika kidato cha sita, limefanya Wakufunzi nao kuelemewa kwani uwiano wa Mkufunzi na Wanafunzi umeporomoka zaidi. Ili kukabiliana na uhaba wa madarasa na walimu imebidi kufundisha programu za mwaka wa kwanza na mwaka wa pili kwa mikondo miwili, asubuhi na jioni. Kwa vile mfumo huu ni mpya umekuwa ni changamoto kubwa ambayo Chuo kinaendelea kuikabili kwa njia mbalimbali.

Hivyo basi Chuo kinaiomba Serikali iendelee kukifadhili katika kupanua miundo mbinu yake hususani katika kumaliza ujenzi wa Kampasi Kuu ya Mloganzila mapema zaidi ili kufanikisha majukumu ya Chuo, kuongeza udahili wa wanafunzi na ubora wa wahitimu wa Chuo hiki.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Pamoja na juhudi nyingi za Chuo za kuboresha mazingira ya mafunzo kazini na kuongeza idadi ya wanafunzi, jitihada hizi haziwezi kuzaa matunda kama changamoto zilizoainishwa katika mpango wa Matokeo Makubwa Sasa hazitafanyiwa kazi. Changamoto hizi ni pamoja na kuboresha mchakato wa ajira na mazingira ya kazi ya wafanyakazi wa sekta ya afya nchini. Tathmini ya hali halisi ya ajira za wafanyakazi wa afya iliyoainishwa katika mpango huu inaonesha kuwa utaratibu wa ajira katika sekta ya afya ya umma una mlolongo mrefu ambao mara nyingi unachelewesha ajira za wafanyakazi hawa. Ucheleweshwaji huu unawafanya wafanyakazi hawa watafute njia mbadala ya kujipatia kipato na hivyo Serikali kupoteza rasimali watu hii muhimu kwenye sekta ya afya.

Aidha tathmini ya mazingira ya kazi iliyofanywa katika mpango huu inaonyesha kwamba, mazingira ya kazi katika sekta ya afya ya umma hayaridhishi hivyo kuongeza uwezekano wa baadhi ya wananchi kuachana na ajira hizo. Hivyo napenda kutoa ushauri kwa Serikali kuangalia upya mpango huu wa ajira kwa wafanyakazi wa sekta ya afya na pia kuboresha mazingira ya kazi katika sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Changamoto za sekta ya afya zinafanana sana na changamoto za utekelezaji wa Matokeo Makubwa Sasa katika taasisi za Elimu ya juu. Kwa sasa mchakato wa kuajiri wanataaluma katika taasisi za elimu ya juu, motisha na mazingira ya kazi hayawavutii watu wenye sifa kujiunga na taasisi hizi. Hii kwa kiasi kikubwa inaathiri mpango wa kurithiana (madaraka) wa wanataaluma (*Faculty Succession Plan*) na hivyo kuathiri ubora wa elimu unaotolewa na taasisi hizi. Hili tatizo linafanya taasisi hizi kushindwa kutoa mchango unaostahili katika kufanikisha Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa wa Elimu ya Juu. Kwa hiyo napenda kutoa ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

1. Kupandisha umri wa kustaafu kwa wanataaluma wa elimu ya juu ili kukabili upungufu uliopo kwa sasa, kama mkakati wa haraka.
2. Kuangalia namna ya kuboresha mchakato wa ajira, maslahi na mazingira ya wanataaluma wa elimu ya juu ili kuvutia wataalam vijana wenye sifa kujiunga na taasisi za elimu ya juu kama mpango wa muda mrefu.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Kwa kumalizia napenda kuwapongeza tena wahitimu wote kwa kufaulu mitihani yao. Nawatakieni kheri na mafanikio katika maisha na shughuli zenu za baadaye. Huko mtakapokwenda kutoa huduma kwa wananchi, nawaomba siku zote mzingatie kauli mbiu ya Rais Wetu Mpendwa, Dr. John Pombe Joseph Magufuliya **"Hapa ni Kazi tu**" kwa kuwahudumia Wananchi kwa uaminifu na uadilifu mkubwa na kwa kujituma. Pia ninyi kwa vile ni Wataalamu wa Fani za Afya wapya *"A new Broom sweeps clean*" mnatakiwa kuonyesha umahiri mkubwa katika kazi zenu, ili muwe mfano wa kuigwa. Mkiwa wataalam wa Afya hodari mtakuwa mnakipa heshima Chuo chenu.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, wageni waalikwa, mabibi na mabwana,
Ahsanteni sana kwa kunisikiliza!

Mwisho

CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI MUHIMBILI

HOTUBA YA MAKAMU MKUU WA CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI – MUHIMBILI; PROFESA EPHATA KAAYA KWENYE MAHAFALI YA TISA YA MUHAS

TAREHE 5 DESEMBA 2015

Mkuu wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili na Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Mheshimiwa Al-Haj Dk Ali Hassan Mwinyi,

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Bw. Deogratias Aloys Ntukamazina,

Katibu Mkuu, Wizara Ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Profesa Sifuni Ernest Mchome,

Katibu Mkuu Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Dk. Donan Mmbado,

Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Muhammad Bakari,

Wajumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili,

Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu na Wakuu wa Vyuo Vikuu Vishiriki Mlioko hapa,

Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika mbalimbali ya Kimataifa,

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Profesa Lawrence Museru,

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Taasisi ya Mifupa Muhimbili, Dk Othman Kiloloma,

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Dk Diwani Msemo,

Viongozi wa Serikali,
Wageni waalikwa,
Maprofesa na Wahadhiri,
Wahitimu,
Wazazi na Walezi,
Jumuiya ya Wanachuo,
Mabibi na Mabwana,

Kwa niaba ya Wanajumuia wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, ninayo heshima kubwa kukukaribisha Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, kwenye mahafali haya ya **tisa** tangu Chuo hiki kiwe Chuo Kikuu kamili. Napenda pia kukushukuru kwa kukubali kuja kuwatunukia stashahada na shahada mbalimbali wahitimu wa mwaka huu.

Aidha napenda pia kuwakaribisha na kuwashukuru wageni waalikwa, viongozi wa Serikali, viongozi wa taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za kiserikali, mabalozi, wazazi, walezi, ndugu na marafiki kwa kukubali mwaliko wa kushiriki nasi katika sherehe hii ya mahafali**. Karibuni sana**.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Awali ya yote, napenda kuungana na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, kumpongeza Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk John Pombe Joseph Magufuli na Makamu wa Rais Mhe Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuongoza Serikali ya awamu ya tano. Pia napenda kumpongeza Mhe Majaliwa Kassim Majaliwa, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa awamu ya Tano, Mawaziri wote walioteuliwa na kipekee Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kuteuliwa na Rais kuongoza wizara hii. Nawatakia baraka za Mwenyezi Mungu katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wahitimu wote wa mwaka huu kwa kufaulu vizuri masomo, licha ya changamoto mbalimbali za kitaaluma na kijamii katika kipindi cha masomo yao. Ni imani yangu kwamba mtakuwa mabalozi wazuri wa Chuo hiki chenye sifa nzuri kitaifa na kimataifa, kwa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa na kuzingatia weledi na miiko ya taaluma zenu.

Mafanikio yaliyofikiwa leo na wahitimu hawa yasingeweza kupatikana bila ya mchango mkubwa wa Serikali, Maprofesa, Wahadhiri, wafanyakazi wote wa Chuo na wafanyakazi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete - Muhimbili, Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Hospitali ya Jeshi Lugalo na wale wa Hospitali na Taasisi nyingine za afya zinazoshirikiana na Chuo katika kuwaandaa wahitimu hawa na kufanikisha siku hii ya leo. Hawa wote pia wanastahili shukrani zetu na pongezi nyingi.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Baada ya kusema hayo, napenda sasa kuchukua nafasi hii kuwatambulisha kwako wahitimu wa mahafali ya leo ambao muda si mrefu utawatunukia shahada ya uzamivu, shahada za uzamili, shahada za kwanza, stashahada za juu na stashahada mbalimbali za Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili.

Mwaka huu wa masomo Chuo kina jumla ya wahitimu **878**, kati ya hao **318** wakiwa ni wahitimu wa kike ambao ni asilimia **36.2** ya wahitimu wote. Azma ya Chuo ni kuwa na asilimia sawa kati ya wahitimu wa kike na wa kiume. Hivyo basi Chuo bado kinaendelea na mpango wake wa kuwawezesha wanafunzi wa kike kujiunga na programu mbalimbali zinazotolewa hapa chuoni.

Aidha katika wahitimu wa mwaka huu, **323** watatunukiwa stashahada na **10** watatunikiwa stashahada za juu katika fani mbalimbali za afya na sayansi shirikishi. Pia wahitimu **351** watapata shahada ya kwanza na wengine **220** shahada ya uzamili. Vile vile wahitimu **11** watatunukiwa Digrii za Uzamili za Utaalamu (*yaani Superspeciality*) na tunao wahitimu **wawili** ambao watatunukiwa shahada za uzamivu.

Ninayo furaha kukufahamisha kwamba katika Mahafali ya mwaka huu mbali na wahitimu kutoka Tanzania, tunao wahitimu kutoka nchi 10 ndani na nje ya bara la Afrika ikiwa ni pamoja na **Burundi,**

Cameroon, Ethiopia, India, Kenya, Malawi, Namibia, Rwanda, Swaziland na Zambia.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Chuo kimeendelea kutekeleza malengo na majukumu yake kupitia Skuli, Kurugenzi na Taasisi zake. Kwa mwaka huu napenda kutaja mambo machache yaliyotekelezwa na Chuo kama ifuatavyo:-

1. Kurugenzi ya Shahada za Awali (*Undergraduate Education*)

Mwaka huu wa masomo wa 2015/16 Kurugenzi ya Shahada za awali imedahili wanafunzi elfu moja na themanini na tano (1085) katika fani mbalimbali, ikiwemo wanafunzi wa shahada ya kwanza 599 na wanafunzi stashahada 586. Hili ni ongezeko la asilimia kumi na tatu (13%) ukilinganisha na udahili wa mwaka jana. Ongezeko hili limetokana na waombaji wenye sifa za kujiunga vyuo vikuu zikiwemo fani za afya na sayansi shirikishi kuongezeka sana na hivyo vyuo vikuu nchini kulazimika kuongeza udahili.

Vile vile, katika jitihada za kukifanya Chuo kiwe na sura ya kimataifa (*Internationlisation*), mwaka huu wa masomo Chuo kina jumla ya wanafunzi kutoka nchi za nje kumi na nne (14) kama ifuatavyo: Burundi, Cameroon, DRC, Ethiopia, India, Kenya, Malawi, Namibia, Rwanda, Swaziland, Sweden, South Sudan, Uganda na Zambia.

2. Skuli ya Tiba

Katika kupanua wigo wa kufundishia wanafunzi kwa vitendo, Chuo kupitia Skuli hii kimeanza utekelezaji wa Mkataba Kati ya Chuo na Jeshi la wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwa kuanza ushirikiano na Skuli ya Tiba ya Lugalo ambayo iko chini ya hospitali ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (TPDF), ya Lugalo jijini Dar es salaam. Pia mchakato wa makubaliano kama haya na hospitali ya Bagamoyo umeshakamilika na hati ya maelewano kati yetu imeshasainiwa. Hati ya Makubaliano kati ya Chuo na Hospitali ya

CCBRT nayo imekamilika na itasainiwa mwezi huu. Inatarajiwa kwamba, utelekelezaji wa makubaliano haya, utapunguza changamoto ya msongamano wa wanafunzi katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili na hivyo kuboresha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wetu.

Kitaaluma, Skuli ya Tiba imeweza kufanya shughuli kubwa ya kugawa (*tailoring)* na kufundisha masomo ya sayansi ya tiba ya msingi (*biomedical sciences*) ili wanafunzi wetu waweze kupata elimu hii kwa kadiri ya matakwa ya shahada husika (*specific degree program requirements*). Utaratibu huu umewezesha kuongeza kiasi cha ufaulu katika masomo haya kwa wanafunzi wetu wa mwaka wa kwanza wa shahada ukilinganisha na miaka ya nyuma.

Vile vile katika mwaka wa masomo 2015/16 Chuo kupitia Skuli hii kimepata udhamini wa "*Seed Global Health*" kwa wanafunzi wanne (4) wa shahada ya uzamili katika fani ya anaesthesiolojia (*MMed Anaesthesiology*). Hii itasaidia kuongeza wataalam katika fani hii ambao wanahitajika sana nchini.

3. Skuli ya Afya ya Kinywa na Meno

Kama alivyoeleza Mwenyekiti wa Baraza, Chuo kinaendelea kubuni mbinu mbali mbali za kuongeza mapato ya ndani. Chuo kupitia Skuli ya Meno kimejikita katika kutoa huduma ya afya ya kinywa kwa wagonjwa. Huduma hii imekuwa chanzo kizuri cha mapato ya ndani hasa baada ya Chuo kuingia mkataba na Shirika la Taifa la Bima ya Afya (*National Health Insurance Fund*). Chuo pia kiko katika mchakato wa kuingia mkataba na mashirika mengine ya bima ya afya ili kupanua wigo wa mapato ya ndani. Hatua za mwisho zimetekelezwa ili kupanua huduma hii kwa kufungua kliniki maalumu ya matibabu ya afya ya kinywa na meno kwa ajili ya wagonjwa wa kulipia (*Private Dental Clinic*).

4. Skuli ya Famasia

Katika kuongeza vyanzo vya mapato ya ndani, Chuo kupitia Skuli hii kimeandaa na kuendesha mafunzo kwa ajili ya watathmini wa ubora wa madawa (*medicine assessors*) kutoka nchi za jumuia ya Afrika Mashariki. Mafunzo haya yatakua endelevu na yanatolewa na Skuli ikishirikiana na Mamlaka ya Taifa ya Chakula na Dawa (TFDA), kupitia kituo chetu cha Ubora wa Utathmini na Usajili wa Dawa katika ukanda wa Afrika Mashariki - RCORE (*Regional Center of Regulatory Excellence*).

Vile vile, Chuo kupitia Skuli hii kiko katika mchakato wa kuboresha maabara yake ili kuijengea uwezo wa kutoa huduma Ustadi wa kupima sampuli za dawa za binadamu (*Proficiency Testing Provider*) kwa ukanda wa Afrika Mashariki. Tunatoa shukrani kwa Shirika la kusimamia viwango la Ujerumani *Physikalish-Technische Bundesanstalt (PTB)* kwa kuisaidia maabara yetu katika mchakato huu. Kwa sasa maabara hii inashiriki katika mashindano ya Ustadi linganifu ambao maabara ishirini (20) kutoka ukanda wa Afrika Mashariki zimeshiriki.

5. Skuli ya Afya na Sayansi za Jamii

Chuo kupitia Skuli hii kwa mara ya kwanza katika, katika mahafali ya mwaka huu, nchi yetu na ukanda huu wa Afrika ya Mashariki na Kusini kimefanikiwa kuwa na wahitimu wa Shahada ya Uzamili katika fani ya Afya ya Mazingira na Kazi (*MSc. Environmental and Occupational Health)*. Shahada ya Uzamili ya Sayansi katika fani ya Afya ya Mazingira na Kazi, inawaandaa wahitimu kuwa na ujuzi na maarifa ya kutosha kukabiliana na changamoto nyingi katika kuhifadhi afya za binadamu na viumbe hai hususani katika mazingira ya kuishi na kufanyia kazi yanayoweza kusababishwa na kemikali, hewa, maji, vyakula na udongo. Wahitimu hawa watakuwa na uwezo wa kutambua, kutathmini, na kudhibiti hatari za afya katika mazingira ya kuishi na

kufanyia kazi. Maeneo ambayo yatanufaika kwa kuwatumia wataalam hawa wa Afya ya Mazingira na Kazi wanaohitimu leo ni pamoja na Vyuo vya Elimu ya Juu, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Afya na Usalama Kazini, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Shughuli za Migodi mikubwa, na Viwanda vikubwa.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Aidha Chuo kupitia Skuli hii kimefanikiwa kukamilisha azma yake ya kuanzisha shahada ya uzamili katika Afya ya Jamii kwa njia ya masafa, yaani *Masters of Public Health (MPH) distance learning* ili kuwafikia Watanzania walio wengi na hasa wa nje ya Dar es Salaam ambao hawawezi kuhudhuria masomo haya hapa chuoni. Kwa awamu hii Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi thelathini na tatu (33) na kinashirikiana na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania katika uendeshaji wa programu hii. Lengo la Chuo ni kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa ili kutoa wataalam wengi zaidi katika fani ya Afya ya Jamii. Mfumo huu pia huwa na gharama nafuu, hivyo kuwezesha mwanafunzi kumudu kujilipia gharama za masomo mwenyewe pindi ufadhili unapokosekana.

Sambamba na hilo Chuo kupitia skuli hii na kwa msaada mkubwa wa Makamu mkuu wa chuo, kimeanzisha progamu ya shahada ya Menejimenti ya Takwimu za Afya, yaani '*Health Information Management Systems*' ikishirikiana na Chuo Kikuu cha *Western Cape* cha Afrika ya Kusini na Chuo Kikuu cha *Applied Sciences Neu-Ulm* cha Ujerumani. Chuo kinaendelea na mpango wake wa kuanzisha programu ya shahada ya uzamili ya Menejimenti ya Huduma za Afya, yaani *MBA Health Services Management* ambayo pia itafundishwa nyakati za jioni kwa lengo la kuwapatia fursa watu wengi kuweza kujiunga na programu hii.

Vile vile kwa mwaka huu, Chuo kupitia skuli hii kimeendesha mafunzo ya kozi fupi za majuma mawili ili kuwajengea wataalam mbalimbali wa afya ujuzi zaidi katika kazi zao na kuboresha ufanisi wa utendaji kazi wao. Kozi hizi ni Kanuni za Msingi za Afya katika eneo la kazi (*Basic Principles in Occupational Hygiene*) pamoja na Menejiment, uangalizi na tathmini ya miradi ya huduma za afya (*Project management, monitoring and evaluation in health care interventions*). Hii pia ni njia mojawapo ya kukipatia Chuo mapato kutokana na vyanzo vyake vya ndani.

6. Kurugenzi ya Masomo ya Uzamili na Uzamivu

Kama Mwenyekiti wa Baraza alivyosema kuhusu umuhimu wa kuongeza wataalam wa afya katika fani mbali mbali ili kufikia malengo ya mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now*), Chuo kupitia kurugenzi hii kinaendelea kuongeza uratibu wa idadi ya wanafunzi wa uzamili na uzamivu na kuongeza uratibu wa programu mpya ikiwa ndiyo kulinganisha faida *(comparative advantage)* kubwa ya Chuo hiki, kulingana na mahitaji ya soko la ajira *(demand driven programs)*. Programu zilizoratibiwa na kuruhusiwa kuanzishwa kwa mwaka wa masomo 2015/2016 ni za Skuli ya Afya na Sayansi za Jamii yaani:-

(i) Master of Science in Health Information Management
(ii) Master of Public Health Distance Learning

Kama nilivyoeleza kwenye hotuba ya mwaka jana, changamoto kubwa kwenye masomo ya uzamili ni ufinyu wa udhamini kwa wanafunzi waliochaguliwa. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ambayo ndiyo ilikuwa mfadhili mkubwa wa programu za uzamili, haiwezi tena kumudu ufadhili peke yake. Kwa mfano Mwaka huu kati ya wanafunzi 547 waliokuwa na sifa na kuchaguliwa kujiunga na Chuo ni wanafunzi 339 (61.9%) wamedahiliwa. Kati ya hawa ni wanafunzi 66 *(19.5% ya walodahiliwa au 12.1% ya waliochaguliwa*) tu ndiyo wamepata

ufadhili wa wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Hii inaonyesha kuwa Wanafunzi wengi wenye sifa na kuchaguliwa kujiunga na Chuo wanashindwa kujiunga kwa sababu ya kukosa ufadhili. Ili kuharakisha kufikia malengo ya taifa ya sekta ya afya kuna umuhimu wa sekta binafsi, watu binafsi na wadau wengine kusaidiana na Serikali katika ufadhili wa wanafunzi hawa wa uzamili.

7. Kurugenzi ya Huduma za Maktaba

Ili kuboresha mafunzo na tafiti na kwenda sambamba na ukuaji wa TEHAMA ulimwenguni, Chuo kupitia Kurugenzi hii kimeendelea kuweka mfumo wa TEHAMA katika huduma zake mbalimbali. Maktaba imeendelea kukusanya na kuingiza taarifa za vitabu, majarida na CDROM kwenye mfumo wa kompyuta ili kusaidia upatikanaji wa haraka wa vitabu hivyo. Kwa sasa jumla ya vitabu 32,341 vimeingizwa kwenye mfumo huu wa kompyuta, na taarifa zake zinapatikana kwenye mtandao kupitia tovuti ya Chuo.

Maktaba ya Chuo imeendelea pia kukusanya na kuingiza taarifa za tafiti mbalimbali zinazofanywa na wanafunzi pamoja na wafanyakazi wa Chuo kwenye mtandao. Kwa sasa kuna jumla ya tafiti zaidi ya 1,344, ambazo ni *theses* na *dissertations*, majarida, ripoti za kitafiti na mada za makongamano ambazo zimeshaingizwa kwenye mfumo wa TEHAMA. Juhudi mbalimbali zinaendelea ili kuwawezesha watafiti wa Chuo kuingiza ripoti za tafiti zao kwenye huu mfumo.

Aidha, kupitia *Bill and Melinda Gates Foundation*, na *Information, Training Center for Africa (ITOCA)*, maktaba imeweza kupata *database* ambayo ina majarida ya sayansi za afya na kilimo zaidi ya 200 ambazo zinapatikana ndani ya chuo bila kupitia mtandao wa Intaneti. *Database* hii inaitwa *The Essential Electronic Agricultural Library* (TEEAL).

Pia, Chuo kupitia Kurugenzi ya Huduma za Maktaba kimeendelea kujiunganisha na database mbali mbali ambazo zinasaidia upatikanaji wa vitabu na majarida kupitia mfumo wa TEHAMA ambazo zinasaidia ufundishaji na utafiti. *Database* hizo zimesaidia upatikanaji wa majarida zaidi ya 14,000 yaani *e-journals* na vitabu 46,000 yaani *e-books*. Database hizo zinaitwa HINARI, AGORA, ARDI and OARE ambazo zinatolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Kilimo (FAO), na Shirika la Mazingira Duniani (UNEP). Chuo pia kimeweza kusaidia upatikanaji wa majarida na vitabu vya kielectronic kutokana na database 29 kupitia Shirikisho la Maktaba za Vyuo Vikuu na Mashirika ya Kitafiti hapa Tanzania (COTUL).

Pia, Chuo kupitia Kurugenzi hii kimekuwa kikiendesha mafunzo mbalimbali kwa wafanyakazi wa chuo, wanafunzi na washiriki wengine kutoka nje ya Chuo. Mafunzo haya hufanya shughuli ya kuandaa machapisho na kuandika ripoti za tafiti mbalimbali kuwa rahisi zaidi. Kwa mwaka wa masomo uliopita, maktaba imeendesha mafunzo ya muda mfupi 12.

8. Kurugenzi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Katika ulimwengu wa leo matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ni kiungo muhimu katika kuboresha utoaji wa huduma. Chuo kupitia Kurugenzi ya TEHAMA kimeendelea kuboresha matumizi ya TEHAMA katika kuboresha utoaji wa huduma na ufanisi. Miundo mbinu, mifumo na huduma za TEHAMA zimeendelezwa ili kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa Chuo na utoaji wa huduma zote muhimu "*core functions*". Chuo kimeongeza kasi ya mtandao wa Intaneti kutoka "*bandwith*" ya Mpbs thelathini (30) mpaka arobaini (*40 Megabits per second)* baada ya kuunganishwa kwenye mkongo wa taifa.

Vile vile Chuo kupitia Kurugenzi hii kimeendelea kutumia mifumo ya habari na mawasiliano ili kurahisisha utendaji, kuendana na mabadiliko ya TEHAMA pamoja na kukabiliana na ongezeko kubwa la wanafunzi. Kurugenzi inatilia mkazo matumizi ya mifumo huru ya habari (*free and open source software system*) ili kupunguza gharama kubwa za kulipia leseni za mifumo ili kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ya fedha za Chuo. Hili linaendana na maagizo ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA).

9. Kurugenzi ya Mafunzo ya Kijiendeleza na Maendeleo ya Uweledi

Chuo kupitia Kurugenzi hii kimeendeleza mkakati wake wa kuratibu na kuendesha mafunzo ya kijiendeleza na warsha mbalimbali (*Faculty Development Workshops*) kwa wakufunzi wa Skuli, Taasisi na Idara mbali mbali hapa chuoni na nje ya Chuo kama vile Chuo Kikuu cha katoliki cha Afya na Sayansi Shirikishi (CUHAS), Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam and Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yosefu (*St Joseph University)*. Kwa mwaka huu Chuo kimeratibu kozi fupi mpya 16 zinazoendeshwa na vitengo mbali mbali hapa chuoni ili kuendana na maendeleo ya sayansi na teknolojia katika sekta ya afya hapa nchini.

Vile vile Chuo kimefanikiwa kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Haile Debas cha Elimu ya Mafunzo kwa wataalam wa fani za Afya (*Haile Debas Centre for Health Professions Education*) ambacho kinatarajiwa kuongeza nafasi na vitendea kazi zaidi katika kutoa mafunzo ya kujiendeleza kwa wafanyakazi ili kufanikisha lengo la kutoa elimu bora kwa wanafunzi wa MUHAS (*preservice*) na kuongeza ufanisi kwa wafanyakazi waliyo kazini katika fani mbali mbali za afya (*in service*). Aidha Kituo hiki kitakuwa na maabara ya kufundisha wanafunzi ili kuongeza umahiri (*Clinical skills Lab*) na vile vile kutoa elimu ya mbali kupitia mtandao (*Distant Learning Education*).

Chuo kupitia Kurugenzi hii pia kimefanikiwa kuendesha kongamano

la tatu la sayansi yaani "*The 3rd MUHAS Scientific Conference*" lililofanyika tarehe 28 hadi 29 mwezi Mei mwaka huu kwa mafanikio makubwa. Kongamano hili lilihudhuriwa na wadau na watafiti takribani 308 kutoka vyuo vikuu mbalimbali pamoja na taasisi za sekta ya afya ndani na nje ya nchi. Jumla ya mada 136 za nyanja mbalimbali za afya ziliwasilishwa na kujadiliwa katika kongamano hilo. Kurugenzi itaendelea kuendesha kongamano hili muhimu ili kutoa fursa zaidi kwa wadau na watafiti wa afya kujifunza, kushirikiana na kubadilishana mawazo kupitia tafiti wanazozifanya.

10. Kurugenzi ya Mipango na Uwekezaji, Kampasi ya Muhimbili

Chuo kupitia Kurugenzi hii kilifanya tathmini ya kwanza ya utekelezaji wa mpango mkakati mpya wa miaka mitano wa Chuo (*Five years strategic plan 2014/15-2018/19*). tathmini hii imeonyesha kuwa Chuo kimeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa pamoja na changamoto zilizopo ikiwemo ukosefu wa fedha. Ili kukabiliana na ufinyu wa ruzuku itokayo serikalini, Chuo kimeendelea kuimarisha vyanzo vya ndani vya uzalishaji mali. Kupitia kurugenzi hii, Chuo kimetengeneza sera ya kuongoza idara mbalimbali Chuoni ili kuongeza mapato ya ndani. Kupitia sera hii kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 Chuo kimefanikiwa kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 4.8 (4,858,027,917) ambayo ni sawa na 65.4% ya lengo lililowekwa. Kurugenzi ikishirikiana na Kamati ya Miradi ya Baraza la Chuo (*Grants Committee of the Council*) inaendelea kuifanyia kazi mipango mbalimbali ya kiuwekezaji itakayoweza kuongeza pato la ndani ili kupunguza utegemezi kwa Serikali.

11. Kurugenzi ya Mipango na Uwekezaji, Kampasi ya Mloganzila

Kupitia Kurugenzi hii Chuo kimeendelea kuratibu uendelezaji wa Kampasi Kuu ya Chuo ya Mloganzila. Ujenzi wa kampasi hii umepewa msukumo wa pekee na umekuwa na mafanikio makubwa mwaka huu.

Miundo mbinu ya barabara, maji na umeme imekamilika kwa awamu ya kwanza kufika sehemu ya Ujenzi kama ilivyopangwa. Ujenzi wa Hospitali ya kufundishia *(Academic Medical Center)* unaendelea kwa kasi kubwa na kwa sasa mkandarasi amemaliza ujenzi wa ghorofa tisa pande zote mbili za hospitali hiyo na yuko katika hatua ya kutekeleza kazi za kumalizia (*finishing works*). Ujenzi unatarajiwa kukamilika mwaka ujao mwanzoni mwa mwezi Juni. Mzabuni wa kuweka vifaa tiba (*medical equipment*) alishaanza kazi yake na vifaa vitaanza kuwekwa hospitalini mwezi Mei mwaka ujao. Aidha, mafunzo yameanza kutolewa kwa wataalam watakaosimamia utendaji kazi wa vifaa tiba ndani ya hospitali.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Ili hospitali inayojengwa iweze kutumika kwa kufundishia na kutoa huduma, ni muhimu kukawa na majengo mengine na miundombinu ya kampasi ya Chuo. Chuo kimetayarisha dokezo sabili (*proposal*) inayoonyesha gharama halisi ya ujenzi wa majengo na miundombinu mingine muhimu. Taarifa hii pamoja na michoro ya awali viliwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya kutafuta fedha za ujenzi. Jitihada mbalimbali za kupata ufadhili wa ujenzi huu zimefanyika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi japokuwa jitihada hizo bado hazijazaa matunda. Ni dhahiri kwamba majengo ya kufundishia ni muhimu ili kuwezesha hospitali inayojengwa kutumika kama ilivyopangwa. Chuo kina imani kuwa Serikali itaendelea na juhudi zake za kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana ili majengo na miundombinu husika yakamilike kwa wakati muafaka.

Kwa sasa, Chuo kimeanza matayarisho kwa ajili ya kuendesha hospitali hii mara itakapokamilika. Kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Yonsei cha Korea Kusini, Chuo kimeanza kutoa mafunzo kwa wataalam wake katika fani mbalimbali zikiwemo uangalizi wa vifaa tiba (*management of medical equipment*), na uendeshaji wa shughuli za hospitali.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Kama nilivyoeleza katika hotuba ya mwaka jana, Serikali ya Tanzania imeridhia makubaliano ya mkopo wa riba nafuu wa Dola za Marekani 9,500,000 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) wa awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kituo cha Ubora cha utafiti, mafunzo na Tiba ya Magonjwa ya Moyo na Mishipa ya Damu katika ukanda wa Afrika ya Mashariki (*Centre of Excellence in Cardiovascular Sciences in East Africa*). Serikali itatoa kiasi cha Dola za Kimarekani 755,000 kwa ajili ya mradi huu. Kituo hiki ambacho kitamilikiwa na Chuo hiki kitajengwa katika eneo la Chuo la Mloganzila sambamba na Hospitali Kuu ya Chuo. Mradi huu ulianza rasmi mwezi Julai 2015.

Katika kutekeleza mradi huu, mpango wa mafunzo (*Training Plan*) kwa wataalam wa fani ya Magonjwa ya Moyo na Mishipa ya Damu, na Mpango wa Manunuzi wa Mwaka (*Annual Procurement Plan*) vimeshaandaliwa na kuidhinishwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Aidha, mchakato wa kumpata mshauri elekezi (*consultant*) wa kuchora na kusimamia ujenzi wa jengo la kituo hiki (*multipurpose building*) umeshaanza. Ujenzi wa jengo hili unatarajiwa kuanza mwezi Juni 2016.

12. Kurugenzi ya Utafiti na Machapisho

Sera ya utafiti na maendeleo (*National Research and Development Policy*) na Sera ya taifa ya Bioteknologia (*National Biotechnology Policy*) za mwaka 2010 zinasisitiza juu ya umuhimu wa utafiti katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kuboresha maisha ya Watanzania. Wito mkuu katika sera hizi mbili ni msisitizo wa kugeuza matokeo yatokanayo na tafiti mbalimbali ili yawe yenye manufaa kwa wananchi. Sambamba na wito huu, utafiti ni moja ya nguzo tatu za Chuo chetu. Kwa kuzingatia umuhimu huu, Chuo kupitia Kurugenzi yake ya Utafiti na Machapisho kwa mwaka huu kimefanikiwa kuratibu miradi ya utafiti zaidi ya 61 inayoendelea hapa Chuoni. Vile vile idadi ya machapisho ya watafiti wa Chuo kwenye majarida ya ndani na

nje ya nchi imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mwaka 2014 mihutasari wa machapisho 495 imechapishwa katika MUHAS *bulletin* ambapo machapisho 308 yametoka kwenye majarida, 168 ni dissertations, 17 yametolewa kwenye makongamano (*conferences*) na machapisho mawili ni ya vitabu. Juhudi zinaendelea kuongeza usambazaji wa matokeo ya tafiti kwa jumuia.

Aidha kwa asilimia kubwa tafiti hizi zinafadhiliwa kupitia wadau wa maendeleo (*development partners*) wa Chuo. Kwa mwaka huu Chuo kina jumla ya wadau wa maendeleo 45 ambao wanakiwezesha Chuo kuendesha tafiti mbalimbali. Kwa mfano Shirika la maendeleo la Sweden-Sida limefadhili tafiti mbalimbali tangu 1986. Tafiti zimekuwa na mchango mkubwa katika kupata ufumbuzi wa matatizo mbalimbali ya afya yanayosumbua jamii ya Watanzania na sehemu nyingine duniani. Kwa hiyo nachukua nafasi hii kuwapongeza watafiti wetu na kuwashukuru wadau wote wa maendeleo. Kipekee nichukue fursa hii kuishukuru Serikali yetu kwa kuweka mahusiano mazuri na wadau wa maendeleo pote duniani ambayo yametuwekea mazingira mazuri ya ufadhili na ushirikiano wa kimataifa katika tafiti. Tunaiomba Serikali iendelee kuunga mkono na kuchangia katika shughuli za utafiti katika nchi yetu kwa ujumla.

13. Kurugenzi Miliki Majengo

Kwa muda mrefu, Chuo kimekuwa kikilipa gharama kubwa za umeme na maji kutokana na kuwa na mita moja iliyounganisha majengo yote yaliyo ndani ya eneo la Chuo. Ili kupunguza gharama za uendeshaji wa Chuo, Chuo kupitia Kurugenzi hii kimefanikiwa kutenganisha mita za umeme kwa matumizi ya nyumba za wafanyakazi, maeneo ya biashara na shughuli za Chuo, kwa kuweka mita za LUKU. Zoezi hili limefanikiwa kupunguza gharama za bili ya umeme kwa takribani ya shilingi milioni ishirini kwa mwezi. Vile vile Kurugenzi hii iko katika hatua za mwisho za kutenganisha malipo ya ankara za bili za maji kati

ya matumizi ya Chuo na maeneo mengine.

14. Kurugenzi ya Rasilimali Watu na Utawala

Chuo kupitia Kurugenzi hii kimeandaa muundo wa uongozi wa hospitali ya kufundishia ya Mloganzila (*Organizational structure*) na muundo wa utumishi kwa wafanyakazi wa hospitali (*Scheme of service*). Tunaishukuru Serikali kwa kuturuhusu kuingiza nafasi za ajira mpya za watumishi wa Hospitali hiyo zipatazo 968 kwenye bajeti ya mishahara kwa mwaka 2015/2016. Tunaomba Serikali itupatie kibali ili tuanze kuajiri watumishi hawa katika mwaka huu wa fedha. Hii ni kutokana na ukweli kwamba watumishi hawa wasipoajiriwa kabla ya Juni 2016, hospitali haitaweza kutumika hata kama jengo na vifaa tiba vitakuwa tayari.

Kutokana na upanukaji wa shughuli za Utafiti, Ufundishaji na Ushauri bado kuna mahitaji makubwa ya watumishi. Tunaishukuru Serikali kwa kuturuhusu kuendelea kuwatumia wanataaluma wastaafu wakiwemo Maprofesa na Wahadhiri Waandamizi. Mpaka sasa Serikali imeruhusu jumla ya Maprofesa na Wahadhiri Waandamizi waastafu wapatao 64 kuendelea kufundisha kwa mkataba. Bila ya wataaluma hawa kuendelea kufundisha, shughuli za kitaaluma zitaathirika kwa kiasi kikubwa hasa ufundishaji wa programu za uzamili na uzamivu. Tunaomba Serikali iendelee kutoa vibali vya kuwatumia wanataaluma hawa hasa kwa wakati huu ambapo Chuo kitaanza kuongeza udahili wa wanafunzi wengi sambamba na ujenzi wa kampasi ya Mloganzila.

13. Taasisi ya Madawa Asili

Chuo kupitia Taasisi yake ya madawa asili kimeendelea kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu na pia huduma kwa jamii. Kwa miaka mitatu mfululizo, Chuo kupitia Taasisi hii kimekuwa kinatoa mafunzo ya kujiendeleza na maendeleo ya Weledi kwa waganga wa tiba asili ili kuboresha huduma kama inavyopendekezwa na sheria ya tiba asili na tiba mbadala ya mwaka 2002, pamoja na miongozo inayotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kanda ya Afrika na maelekezo ya sera ya Afya ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ya mwaka 1990.

Chuo kwa kupitia taasisi hii kimeendelea na juhudi za kapanua wigo wa ushirikiano kati ya taasisi za ndani na nje ya nchi. Kwa mwaka huu Chuo kimesaini makubaliano na Chuo Kikuu cha Kyung Hee, Korea ya Kusini kwa lengo la kubadilishana utaalam wa kufundisha utengenezaji wa dawa za asili.

14. Taasisi ya Sayansi Shirikishi za Afya

Chuo kupitia Taasisi ya Sayansi Shirikishi za Afya kimeendelea kutoa mafunzo ya jioni katika fani mbalimbali. Fani hizi ni pamoja na Diploma ya Sayansi za Ufundi Maabara ya Tiba, Diploma ya Sayansi za Afya ya Mazingira, Diploma ya Radiografia ya Uchunguzi wa Magonjwa, Diploma ya Uuguzi na Diploma ya Sayansi za Famasia. Hii imesaidia kutoa fursa kwa wafanyakazi kusoma huku wakiendelea na utumishi katika kazi zao. Uwepo wa mafunzo hayo licha ya kusaidia kuongeza wataalam wa afya nchini, pia ni chanzo cha mapato ya ndani.

Chuo kupitia Taasisi hii kimepanga kuongeza programu mpya tatu ambazo ni Diploma ya Kumbukumbu za Afya, Diploma ya Mazoezi ya Viungo (*Physiotherapy*) na Diploma ya Magonjwa ya Macho. Watalaam hawa wanahitajika sana nchini na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Kwa kumalizia napenda kuwapongeza tena wote wanao hitimu leo na kuwatakia mafanikio mema katika shughuli zenu mtakazoenda kuzifanya za kujenga taifa. Hongereni sana na ni matumani yangu kwamba wengi wenu mtarudi tena hapa Chuoni kwa ajili ya masomo ya juu zaidi ili kujiongezea ujuzi na weledi katika fani zenu. Kama ilivyo kawaida tunategemea mtaendelea kuwa mabalozi wazuri wa Chuo hiki, popote pale mtakapokuwa.

Mwisho kabisa naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa wanataaluma wote na wafanyakazi wengine wa Chuo hiki kwa kushiriki kikamilifu na kuhakikisha kwamba wanafunzi hawa wanaohitimu na wengine wote wa Chuo hiki wanapata elimu itakayowawezesha kutekeleza majukumu yao huko waendako.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, wageni waalikwa, mabibi na mabwana,

Asanteni kwa kunisikiliza na nawatakieni maadhimisho mema ya Krismasi na Mwaka Mpya wa 2016.

MWISHO

05 Desemba, 2015